# KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU (LHRC)

## MAONI YA KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU KUHUSU

## MKATABA WA USHIRIKIANO WA KIUCHUMI NA KIJAMII KWA AJILI YA UENDELEZAJI NA UBORESHAJI WA UTENDAJI KAZI WA BANDARI TANZANIA KATI YA SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA NA SERIKALI YA DUBAI

Juni 13, 2023

## A. Utangulizi

**Ufuatao ni uchambuzi wa LHRC** kuhusu Mkataba wa Ushirikiano wa Kiuchumi na Kijamii kwa ajili ya uendelezaji na uboreshaji wa utendaji kazi wa Bandari Tanzania kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Ufalme wa Dubai.

Uchambuzi huu umefanywa kwa mtazamo wa haki za binadamu kama ilivyoainishwa katika Mkataba wa Haki za Kiraia na Kisiasa, 1966 pamoja na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 na kutoa mapendekezo yake. Msingi wa uchambuzi huu ni uwazi, uwajibikaji na dhana ya ushiriki na ushirikishwaji wa wananchi katika mambo yanayowahusu wao wenyewe na rasilimali zao kama ilivyoainishwa katika ibara ya 18 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977, pia ibara ya 8 ya Katiba hiyo.

LHRC inaendelea kuweka msisitizo katika dhana ya uhuru wa kupata taarifa kama ilivyoainishwa katika ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 ambayo inaainishwa haki ya kila mtu kuwa na uhuru wa kutafuta, kupokea na kusambaza taarifa.

**Ndugu waandishi wa Habari,**
Mnamo tarehe 05 Juni 2023, ilisambaa taarifa katika mitandao ya kijamii kutoka ofisi ya Katibu wa Bunge juu ya mwaliko kwa umma wa kutoa maoni kuhusu Azimio la Bunge.
Azimio kuhusu mapendekezo ya kuridhia makubaliano kati ya serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Dubai kuhusu ushirikano wa kiuchumi na kijamii kwa ajili ya uendelezaji na uboreshajiwa utendajii kazi wa bandari Tanzania la mwaka 2023.

Mwaliko huo uliainisha tukio la kupokea maoni kuwa ni siku ya Jumanne ya tarehe 06 Juni, 2023 saa saba na nusu mchana katika ukumbi wa Msekwa D ofisi ya Bunge, Jijini Dodoma. Barua ya mwaliko ilichapishwa kwenye tovuti ya Bunge pamoja na mitandao rasmi ya ofisi ya bunge.

Hata hivyo, kuna masuala kadhaa kuhusu mkataba huu yamezua mjadala katika majukwaa mbalimbali. Masuala hayo ni pamoja na muda wa mkataba na uvunjaji na ukomo wa mkataba. Hivyo basi, LHRC iliona kuna haja ya kufanya uchambuzi wa kisheria wa mkataba huo na kutoa maoni kuhusu baadhi ya vifungu.

**B. Maoni ya LHRC ni kama ifuatavyo;**

**1. Aina ya uwekezaji**

Mkataba haujainisha umiliki wa Serikali ya Tanzania au wananchi wake katika uwekezaji huo, hivyo kutokuwa bayana kwa aina ya umiliki kunaleta tafsiri na mwanya wa kutokuwepo kwa fursa kwa wananchi wa Tanzania kumiliki sehemu ya uwekezaji huo moja kwa moja kwa njia ya kununua hisa au kupitia umiliki wa Serikali.

**2. Kampuni moja kupewa wigo mkubwa wa uwekezaji**

Ibara ya 2 ya Mkataba inaweka lengo la kuingia makubaliano yenye nguvu ya kisheria kufanya ushirikiano ya uendelezaji, uboreshaji na uendeshaji wa maeneo mbalimbali ikiwemo, bandari za baharini na maziwani, maeneo maalum ya kiuchumi (EPZ), maeneo makubwa ya kuweka mizigo na kanda za kibiashara na maeneo mengine ya kimkakati yanayohusu miundombinu ya bandari.

Tafsiri ya ibara ya 2 inaweza kuhusisha Bandari ya Dar es Salaam, Bandari Tanga, Bandari ya Mtwara, pamoja na Bandari ndogo ya Kipumbiwi, Bandari ya Kagombe, Bandari Mkwaja, Bandari ya Lindi, Bandari ya Kilwa Masoko, Bandari ya Mafia, Bandari ya Bagamoyo na Bandari ya Pangani, Bandari ya Mwanza, Bandari ya Kemondo, Bukoba na Bandari ya Musoma.

LHRC ina maoni kwamba, wigo na upana wa maeneo ya uwekezaji ni mkubwa mno, ikizingatiwa ya kwamba, Mamlaka ya Bandari Tanzania inaendesha bandari kubwa zaidi ya 30 za baharini na maziwa makuu.

Pamoja na majibu ya Serikali kupitia Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Profesa Makame Mbarawa kuwa, si bandari zote zitahusika moja kwa moja katika uwekezaji huo, ila ni hadi pale Serikali ya Tanzania itakapomtaarifu mwekezaji

kuhusu fursa za uwekezaji kama ilivyoainishwa katika Ibara ya 4 (2) ya mkataba, bado majibu hayo si yenye kujitosheleza kwa kuwa lengo la msingi la mkataba huo ni kufanya uwekezaji katika bandari zilizo chini ya Mamlaka ya Bandari (TPA).

### 3. Mchakato wa manunuzi

Ni wazi kuwa, bado kuna sintofahamu kutoka kwa wananchi kuhusu kufuata taratibu za mchakato wa manunuzi kama inavyohitajikwa kwa mujibu wa Sheria ya Manunuzi ya Umma Namba 9 ya 2011.

Kwa mujibu wa kifungu cha 64 cha Sheria hiyo, inaainisha kuwa, taasisi yoyote ya umma inayotaka kufanya mchakato wa manunuzi inapaswa kutumia utaratibu wa ushindani kwa mujibu wa sheria. Ushindani huu unamaanisha kushindanisha kwa wazi taasisi zaidi ya moja na hatimaye kuchagua moja.

Tofauti na mchakato huu wa kupata mwekezaji *DP World* hakuna uwazi wa namna ya mwekezaji huyu alivyopatikana. Utaratibu wa kufanya *single sourcing* unaruhisiwa kwa sheria ikiwa tu, hakuna mwekezaji mwingine yoyote anayeweza kutoa huduma hiyo; kuna uharaka sana wa kutekeleza jambo husika kupitia mtoa huduma huyo; kuna hitaji la ulinzi na usalama wa Taifa wa kumtumia mtoa huduma huyo.

### 4. Faida inayoratajiwa kupatikana kwa kuingia mkataba huo

Kwa upande mwingine, mkataba haujaweka wazi, faida ambayo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itapata mara baada ya kuanza kwa utekelezaji wa mkataba huo. Jambo hili, linaongeza hofu ya kuingia mkataba huu kwa kuwa hakuna mahali ndani ya mkataba unapoonesha matarajio ya faida itakayopatikana kila mwaka kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pia thamani ya jumla ya utekelezaji wa mkataba huo.

Kumekuwa na mijadala kuwa ni ngumu kwa thamani halisi kufahamika katika mkataba huu kwa kuwa kutakuwa na mikataba mingine ya utekelezaji, ni maoni yetu kuwa kwa kuwa mkataba huu unaweka msingi kwa mikataba yote ya

utekelezaji basi mikataba ya uwekezaji nayo iwekwe wazi ili umma uweze kujua thamani ya uwekezaji katika mradi huu.

Hivyo kutokuwa na msingi madhubuti kuhusu faida inayotarajiwa kupatikana katika utekelezaji wa mikataba hiyo ni dosari mojawapo ya kisheria ambayo imejenga hofu kwa wananchi. Kwa mujibu wa **kifungu cha 25** cha Sheria ya Mikataba Sura Namba 345 ambacho kinaainisha kuwa, makubaliano bila ya faida tarajiwa *"consideration"* ni batili mbele ya sheria. Hivyo, ni wazi kuwa mkataba huu haujaweka bayana faida tarajiwa kuhusu mkataba huo.

5. **Ibara ya 6 Sharti la Mwekezaji kutoingiliwa kwa sababu zozote**

Inaweka takwa la Serikali ya JMT kuhakikisha kampuni ya uwekezaji inapata vibali, haki ya kutumia ardhi na motisha za kiuwekezaji kwa ajili ya utekelezaji wa mkataba wa mradi kwa mujibu wa sheria. Pia ikiwa DPW or kampuni itakayotekeleza mradi ikiomba Serikali ya JMT kuzuia vitendo ambavyo ni kinyume cha sheria ila vitakuwa halali kwa sababu za kiusalama kama inavyoweza kueleweka na nchi hizo mbili.

Changamoto ya kifungu hiki, ni pale ambapo kitendo chochote kitakachofanyika kwa sababu za kiusalama kinaweza kisipokubaliwa na upande DP World kinaweza leta utata wa kisheria na hivyo kusababisha mgogoro utakahitaji usuluhishi. Hivyo, DP World inatakuwa imejiweke sehemu salama kwa kuwa kitendo hicho kwa mujibu wa ibara ya 6 (2) haileweki au kukubalika na DP World.

6. **Ibara ya 9 na 18 suala ya motisha na kikodi**

Vipengele hivi vinaainisha masuala ya kikodi, ushuru wa forodha na makato mengine yatakayofanywa kwa mujibu wa sheria, hata hivyo kipengele hiki kinatoa mwanya kwa Serikali kutoa motisha kwa mwekezaji wakati mkataba huu haitaji aina au kiwango cha motisha hiyo. Pamoja na kuwepo kwa kipengele cha motisha hiyo kutolewa katika mikataba mingine ya utekelezaji wa miradi (Host Governments Agreements "HGAs) iliyotajwa katika mkataba mkuu.

LHRC inapendekeza kuwa mikataba ya utekelezaji iainishe ukomo wa juu na wa chini wa motisha hizo zitakazotolewa katika mikataba mingine ya utekelezaji ili kuepuka kutumika vibaya kwa kipengele hiki wa baadhi ya

watendaji wa Serikali wasiyo waaminifu. Kwa kuwa, wanaweza kutoa misamaha ya kodi na nafuu nyingine kwa kadri wanavyoona inafaa. Na mikataba hiyo iwekwe wazi kwa kuwa ndani ya mkataba mkuu motisha haijabainishwa.

7. **Ibara ya 20 (2) (e) Utatuzi wa migogoro**

Endapo kutatokea mgogoro baina ya pande mbili, yaani Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kampuni ya Uwekezaji, mgogoro huo utataliwa na vyombo vya usuluhi wa migogoro nchini Johannesburg, Afrika ya Kusini.

LHRC inaungana na kifungu hiki kwa kuwa kinaendana na **Sheria za Kimataifa za Uwekezaji**, **Sheria ya Utatuzi wa Migogoro Sura Na.15, 2020** pamoja na **Sheria ya Uwekezaji, 2022** kwa kuwa inaendana sheria hizo. Hata hivyo kipengele hiki kinapingana na kifungu cha 11 cha Sheria ya Ulinzi wa Rasilimali za Umma Namba 5 ya mwaka 2017 kinachotaka migogoro yote ya uwekezaji isikilizwe na Mahakama ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

8. **Ibara ya 23 Muda na Ukomo wa Mkataba**

Mkataba haujaweka bayana kipindi mahususi cha utekelezaji wa mkataba huo kama ilivyo katika misingi inayoongoza uendeshaji wa mikataba ya kimataifa, moja wa msingi huo ni muda na ukomo wa mkataba. Ibara ya 23 haiko bayana kuhusu ukomo mahususi wa mkataba huo, badala yake inaweka mazingira yatakayopelekea kukoma kwa mkataba ikiwemo; kusitishwa kabisa kwa miradi yote ya kimkataba; pamoja na kuisha kwa mikataba ya utekelezaji wa miradi.

Hata hivyo, ibara ya 23 (2) inaweka **sharti la kuendelea kwa mkataba** hata baada ya kusitishwa kwa mkataba huo, kwa hoja ya kuwa mkataba huo umesitishwa nje ya muda. Hivyo ni wazi kuwa mkataba umeweka masharti magumu ya usitishwaji wake.

Ni muhimu kuwepo kwa kipindi maalumu cha ukomo wa mikataba ya utekelezaji ili kutoingia kwenye utata wa kisheria uliyopo katika ibara ya 23 ya mkataba mkuu.

Ibara ya 23 (4) inaweka katazo la nchi moja kujitoa katika mkataba huo katika mazingira yoyote yanayohusu uhusiano baina ya nchi mbili hata pale pande yeyote inavunja mkataba husika. Kifungu hiki kinamaanisha mkataba huu ni wa kudumu maisha yote na na hakuna namna ya kujitoa au kuuvunja.

**9. Ibara ya 30 Uimara wa Mkataba**

Kipengele hiki kinaweka mazingira ya kutoyumbisha uendeshaji wa mkataba huu. Hata hivyo, kifungu hiki hakijaweka bayana aina ya mazingira ya kuweka uimara wa mkataba huo. Hivyo, hii inatoa mwanya kwa mikataba ya utekelezaji kuweka mazingira hayo ambayo pengine wananchi wanaweza wasiyaone.

**C. Mapendekezo ya nini kifanyike**

Mapendekezo ya LHRC yamejikita katika msingi wa kifungu cha 22 cha mkataba kinachoruhusu marekebisho ya mkataba pale itakapohitajika, mapendekezo yetu ni kama ifuatavyo;

1. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kurejea upya vipengele vya mkataba vyenye changamoto ya kisheria, hususani vile ambayo vilivyoibua mjadala mkubwa kwa wananchi. Hii inaweza kufanyika katika hatua za mapema kwa msingi wa hoja zilizoibuliwa na wananchi wakati kuhusu mkataba huo.
2. LHRC inapendekeza kurekebishwa kwa mkataba huo ili kuweka wazi wazi mazingira yatakayoweka uimara wa mkataba *"Stabilization Clause",* mathalani kama ni mazingira ya kikodi ni muhimu yaianishwe bayana ili kuepeka mchakato wowote utakaoweza kutumia mwanya huo kwa maslahi binafsi na kuumiza maslahi ya umma.
3. LHRC inapendekeza kuwekwa wazi kiwango cha umiliki wa sehemu ya uwekezaji huo ili wananchi kufahamu faida itakayopatikana katika uwekezaji huo husasani katika mikataba ya utekelezaji wa mradi.

**Mwisho,** ni vema kuendelea kwa ari ya uwazi wa mikataba ya kiuwekezaji inayohusu maslahi mapana kwa Taifa kama ilivyojitokeza katika mkataba huu

kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na DP World. Dhana hii inakwenda sambamba na misingi ya *Open Government Partnership (OGP)* ambayo ni; uwazi, uwajibikaji na ushiriki mpana wa wananchi.

Pia tunapendekeza kuwepo na ushirikishwaji mpana wa wananchi kwani mkataba huu uliopitishwa na Bunge tarehe 10 June 2023 haukuwa na ushirikishwaji wa kutosha.

LHRC inaungana na watanzania wote wenye mapenzi mema na nchi yao kwa kuhamasisha ushiriki wa shughuli zinazoleta ukuaji wa uchumi
Pia, kwa kipekee, LHRC inaamini kuwa uwekezaji wenye tija husaidia Taifa kujikomboa katika dimbwi la umasikini na hatimaye taifa kujitegemea na kuwa na wananchi wenye maisha bora na maendeleo.

**Kuhusu kesi za DP World dhidi ya nchi mbalimbali**

Kutokuwepo kwa ushindani ni moja ya hofu ilitanda katika jamii, kwa kuwa kuna taarifa kadhaa zinazohusu kampuni ya DP world na kesi ilizoshitaki nchi iliyoingia nazo mikataba kama ifuatavyo;


**Jedwali la kesi za uwekezaji**

| Na. | Baadhi ya kesi za kiuwekezaji kati ya DP World nchi mbalimbali |
|---|---|
| 1. | DP World dhidi ya Djibouti (2021). ICSID<br>DP World ilishinda kesi dhidi ya Djibouti. DP World ilikuwa ikitafuta fidia kwa madai ya kwamba Djibouti ilikukiuka mkataba na kunyang'anywa bandari ya Djibouti, Doraleh na kuwapa Kampuni ya uwekezaji ya china.<br>Djibouti iliamriwa kulipa dola za kimarekani milioni 533 kwa kuvunja masharti ya mkataba. |
| 2. | DP World dhidi ya Pakistan (2020). ICSID ilitupilia mbali kesi iliyoletwa na DP World dhidi ya Pakistan. DP World ilikuwa ikitafuta fidia kwa madai ya kukiuka mkataba na kunyang'anywa mali na Pakistan. |

| | |
|---|---|
| 3. | DP World dhidi ya Argentina (2018). ICSID ilitupilia mbali kesi iliyoletwa na DP World dhidi ya Argentina. DP World ilikuwa ikitafuta fidia kwa madai ya kukiuka mkataba na kunyang'anywa mali na Argentina. |
| 4. | DP World dhidi ya Peru (2015). ICSID ilitupilia mbali kesi iliyoletwa na DP World dhidi ya Peru. DP World ilikuwa ikitafuta fidia kwa madai ya kukiuka mkataba na kunyang'anywa mali na Peru. |

**Imetolewa leo Juni 13 2023 na;**

**Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC)**



**Dr. Anna Henga**
**Mkurugenzi Mtendaji**